## HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI

## TAARIFA FUPI YA MAENEO YANAYOFAA KWA AJILI YA UWEKEZAJI KATIKA SEKTA MBALIMBALI

### UTANGULIZI

### MIPAKA

Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ipo kati ya Latitudo nyuzi 5.30 na Longitudo 7.34 Mashariki mwa mstari wa Green Wichi. Halmashauri ya Wilaya imepakana na Wilaya na Mikoa kama ifuatavyo:-

Mashariki---------------------Wilaya ya Bahi Mkoa wa Dodoma

Magharibi- -------------------Halmashauri ya Wilaya ya Itigi

Kaskazini---------------------Wilaya ya Ikungi Mkoa wa Singida

Kusini Mashariki------------Wilaya ya Iringa Mkoa wa Iringa

Kaskazini Mashariki--------Wilaya ya Chemba Mkoa wa Dodoma

### ENEO

Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ina kilometa za mraba 14,118 ambazo ni sawa na asilimia 28.6 ya eneo lote la Mkoa wa Singida wenye ukubwa wa kilometa za mraba 49,341.Kilometa za mraba 7,650 ni eneo la Hifadhi za (Rungwa, Muhesi na kizigo), eneo linalofaa kwa kilimo ni kilomita za mraba 847, eneo la malisho ni kilomita za mraba 1,835, eneo la misitu ya vijiji ni kilomita za mraba 3,645 na eneo la makazi ni kilomita za mraba 141.18.

### IDADI YA WATU

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ilikuwa na wakazi wapatao 296,763, wanaume 146,030 na wanawake 150,733. Aidha kiwango cha ongezeko la watu ni asilimia 3.7. Kwa mujibu wa maoteo ya Idadi ya Watunya mwaka 2016 Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni inakadiriwa kuwa na wakazi wapatao 213,010, wanaume 104,375 na wanawake 108,635. Upungufu wa idadi ya wakazi kutoka mwaka 2012 ukilinganisha na 2016 inatokana na kuundwa kwa Halmashauri mpya ya Itigi.

## ENEO LA UTAWALA

Kiutawala Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ina Jimbo Moja la Uchaguzi ambalo ni Jimbo la Manyoni Mashariki, Tarafa 4 (Nkonko, Kintinku, Kilimatinde na Manyoni), Kata 19, Vijiji 58 , Vitongoji 258 na Mamlaka ya Mji moja ambayyo inafahamika kama Mamlaka ya Mji Mdogo wa Manyoni ambao una kata 3 na Vitongoji 30.

## HALI YA HEWA KWA UJUMLA

### HALI YA MVUA

Mvua hunyesha kwa wastani wa milimita kuanzia 500-700 kwa mwaka. Kwa kawaida mvua huanza kunyesha kuanzia mwezi December mpaka March. Kuanzia mwezi April mpaka Novemba ni kipindi kirefu kisichokuwa na mvua.

### HALI YA JOTO

Hali ya joto kwa kawaida inatofautiana kulingana na mwinuko kutoka sehemu moja hadi nyingine. Hata hivyo wastani wa joto huanzia nyuzi joto 20 kwenye mwezi Julai hadi nyuzi 30 kwenye Mwezi Octoba.

### HALI YA UPEPO

Upepo kwa kawaida huvuma kwa mwendo kasi wa kuanzia 95km kwa siku sawa na wastani wa mita 1.1 kwa sekunde, hata hivyo wastani wa upepo kwa mwaka ni 140km kwa siku katika mwezi Septemba na km 53km kwa mwezi Februari. Upepo unaovuma kwa mwendokasi uanozidi 100km kwa siku na wastani wa mita 1.2 kwa sekunde ni kwa miezi ya Agosti hadi Desemba.

## HALI HALISI YA UOTO WA ASILI NA UDONGO

Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni imegawanyika katika kanda tatu za maeneo ya Kilimo:-

(**a)Bonde la ufa**-Hili ni eneo lenye watu wachache lakini likiwa na wafugaji wengi wa ng'ombe. Hili eneo kwa kawaida hupata mvua kidogo kuanzia wastani wa milimita

Hili ni eneo ambalo lipo upande wa Magharibi mwa Wilaya na hupata mvua  kuanzia 500-650mm kwa mwaka. Udongo wa eneo hili ni tifutifu uliochanganyika na kichanga,udongo wa mfinyanzi ulio mweusi ambao hupasuka wakati wa jua. Aidha mazao yanayolimwa ni Mahindi, Mtama, Alizeti, Ufuta, Uwele, Mpunga, Karanga, Mihogo na Maharage.

### (b)Eneo la Uoto wa Miombo

Udongo wa eneo hili ni tifutifu uliozidiwa na kichanga.Eneo hili hupokea mvua kanzia wastani wa milimita 500 hadi 700 kwa mwaka.Idadi ya mifugo inayofugwa katika maeneo haya ni kidogo kutokana na mbungo waliopo kwa baadhi ya maeneo. Mazaao yanayolimwa katika maeneo haya ni Mahindi, Mtama, Uwele, Mihogo, Viazi Vitamu na Karanga. Aidha baadhi ya Maeneo hujihusisha na shughuli ya ufugaji wa nyuki na uwindaji.

### (c)ENEO LILILOINUKA

Eneo hili kwa kawaida huwa lina mvua isiyotabirika ambayo hunyesha kuanzia milimita 550-600 kwa mwaka. Maeneo yanayohusika na ukanda huu ni eneo la Kaskazini ya Manyoni. Eneo hili lina udongo aina ya asidiki na tifutifu iliyochanganyikana kichanga.

**FURSA ZA UWEKEZAJI**

## 1: SEKTA YA KILIMO NA UMWAGILIAJI

Katika Sekta ya Kilimo maeneo yanayofaa kwa ajili ya uwekezaji na kama ifuatavyo:-

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Upatikanaji wa eneo linalofaa kwa kilimo lenye ukubwa wa Hekta 7053 kwa ajili ya uzalishaji wa zao la Alizeti. | i) Kujenga kiwanda cha kukamua mafuta ya<br><br>Alizeti (medium scale)<br><br>ii) Mwekezaji anaweza kujenga kiwanda cha kuchuja mafuta ya Alizeti Double Refainary<br><br>iii) Mwekezaji anaweza kutengeneza vifungashio vya kufungashia mafuta ya Alizeti | i) Wakulima watauza mazao yao kiwandani kwa bei nzuri<br><br>ii) Thamani ya mazao itaongezeka kwa kuongeza kipato katika familia<br><br>iii) Upatikanaji wa ajira. | |
| 2. | Upatikanaji wa Hekta 5200 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji wa zao la mpunga. | Kufungua mashamba ya kilimo cha umwagiliaji katika zao la mpunga katika maeneo ya Chikuyu, Msemembo, Saranda, Udimaa, Mtiwe, Ngaiti, Maweni, Chikola na Chibumagwa. | Wakulima wataondokana na baa la njaa | |

## 2: SEKTA YA MIFUGO

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Eneo linalofaa kwa ufugaji wa Ng’ombe wa nyama na maziwa, kuna jumla ya ekari 11,860 Mkwese kwa ufugaji wa Ng’ombe wa kisasa na kienyeji | Kiwanda cha nyama kinaweza kuanzishwa. Aidha Hali ya Hewa na eneo linalofaa kwa malisho na maji kwa ufugaji wa Ng’ombe wa kisasa na kienyeji. Pia shughuli za unenepeshaji wa mifugo | Ajira zitapatikana kwa kuanzisha Kiwanda cha Nyama na kutakuwa na soko la uhakika | |

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| | | unaweza kufanyika | | |
| 2. | Kuna banda la kusindika ngozi huko Kipondoda. Machinjio ya Manyoni inachinja wastani wa Ng'ombe 10 na mbuzi 4 Kila siku. Aidha zipo mashine za kutengeneza bidhaa za za ngozi. | Uzalishaji wa ngozi za Ng'ombe na Mbuzi unaozalishwa kila siku. Unaweza kusindika ngozi na kupata ngozi zilizosindikwa (Leather) kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali za ngozi kwa kutumia mashine zilizopo kwa njia za vikundi vya akina mama na vijana | Kupatikana ajira kwa vikundi vya kutengeneza na kuuza bidhaa za ngozi. Aidha viatu vina soko kubwa kwenye mashule yetu ya Msingi na Sekondari | |
| 3. | Kuna Eneo la Halmashauri ya Manyoni jumla ya Hekta 150 Saranda linalofaa kwa ufugaji wa Mbuzi | Kuanzisha shamba la mbuzi kwa ajili ya unenepeshaji na uzalishaji | Upatikanaji wa ajira | |

## 3: SEKTA YA MADINI

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA |
|---|---|---|---|
| 1 | Wilaya inayo maeneo yanayofaa kwa ajili ya uchimbaji wa Madini ya dhahabu kama vile Iruma katika Kata ya Sasilo, Londoni katika Kata ya Makuru, na uchimbaji wa madini ya Uranium katika kijiji cha Mitoo Kata ya Manyoni. | Makampuni ya uchimbaji madini yanaweza kuwekeza katika kuchimba madini katika maeneo ya Londoni na Iruma kwa kushirikiana na Wananchi au kwa njia ya ubia au uchimbaji wa moja kwa moja | -Wananchi wanaweza kuingia ubia na wawekezaji katika uchimbaji wa madini<br>-Wananchi wanaweza kusaidiwa teknolojia ya uchimbaji.<br>-Maeneo ambayo hupatikana madini yanaweza kunufaika kwa kupatiwa huduma bora za kijamii.<br>-Halmashauri kwa upande wake inaweza kupata mapato ya ndani kama mrahaba wa madini yanayopatikana. |

**4: SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA**

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kupata wawekezaji watakaowekeza kwenye nyumba kwa kujenga nyumba za makazi mfano NHC, NSSF n.k | Wilaya ya Manyoni kwa sasa inakuwa kwa kasi, hii ni kutokana na Makao Makuu ya Nchi kuwa Dodoma ni matarajio yetu kuwa na maendeleo makubwa zaidi kwani mji huu utakuwa na wageni wengi na sio wote watakaopenda kukaa kwenye nyumba za wageni kutokana na gharama kuwa kubwa, pamoja na kuwasaidia watumishi wanaohamia na ambao hawamiliki nyumba | Uchumi wa Wilaya utakuwa kwa kasi na kusaidia wananchi wake kuishi maisha ya kiwango cha kati | Wawekezaji wapewe maeneo ya kuwekeza pindi wanapoomba Maeneo yaliyopo pembezoni mwa Mji |
| 2 | Kujenga viwanda vya kusindika mazao ya chakula kwa kuwa mazao hayo yanalimwa kwa wingi katika Halmashauri hii kwani maeneo ya mbuga yanapatikana kwa wingi yanayofaa kwa shughuli za kilimo | Wawekezaji wanaweza kujenga Viwanda vya Kusindika Mazao kama Alizeti, Ufuta, Mahindi na Karanga ili kuongeza thamani za mazao kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao hayo katika maeneo ya Halmashauri yetu, pia mwekezaji anaweza kulima mashamba makubwa kwa ajili ya kuongeza uzalishaji zaidi | Kuinua kipato kwa mwananchi au mkulima mdogo ili kuondoa umaskini | Wawekezaji wapewe maeneo ya kuwekeza pindi wanapoomba |

**5: SEKTA YA MALI ASILI NA UTALII**

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Eneo la misitu kwa ajili ya ufugaji wa nyuki na | -Wawekezaji wanaweza kutumia vichaka | -Kupata fedha za kigeni kupitia | |

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| | uwindaji. Eneo la misitu ni 25.8% ya eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni | vilivyopo kwa kufuga nyuki na kujipatia asali iliyo bora<br>-Uwindaji wa kitalii ambao unaweza kufanyika kupitia uwepo wa Vitalu vya uwindaji wa kitalii katika Mapori ya akiba ya Rungwa, Muhesi na kizigo | Uwindaji wa Kitalii | |

**6: SEKTA YA ELIMU**

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Elimu Sekondari**<br>Upatikanaji wa eneo lenye ukubwa wa Hekta 10 Kata ya Muhalala. kwa ajili ya ujenzi wa Shule na taasisi nyingine za kielimu. | -Mwekezaji anaweza kujenga Shule ya Sekondari yenye Kidato cha I-IV kutokana na Kata hiyo kutokuwa na Shule ya Sekondari. Aidha Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni ina Shule moja tu ya A-Level ambayo ni ya Serikali kwa kuwa wafanyakazi wengi wa kutoka ndani na nje ya nchi wanategemewa kuja kuishi ama kufanya kazi na familia zao.<br><br>-Hivyo ipo haja eneo hilo liandaliwe na watu wa mipango ili kama shule nyingine ikijengwa isaidie kuondoa msongamano wa wanafunzi kwenye Shule za Kata ya Manyoni Mjini | i) Shule itatoa Elimu kwa wenyeji na wageni<br><br>ii) Wafanyakazi wageni wa Taasisi zilizotajwa watakaa au kufanya kazi karibu na watoto wao wanaosoma<br><br>iii) Kupunguza umbali wa kuhudhuria Shule zilizo nje ya Kata<br><br>iv) Wafanyakazi wanaoishi Manyoni wanaweza kuja na wanafunzi wao na baada ya kazi wakarudi nao; mfano madereva, mama lishe na mafundi<br><br>v) Mpango wa kila Kata kuwa na Sekondari utakuwa | Ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Magari, Mizigo na Sehemu ya Kuegesha magari ukikamilika kujengwa Muhalala itapelekea kuwa na ongezeko kubwa la watu na hitaji la upanuzi wa huduma za Elimu |

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| | | | umetimia<br><br>vi) Ongezeko la Ajira/Kipato<br><br>vii) Kupunguza “Drop Out” ya wanafunzi wa Shule za Kata ya Manyoni Mjini wanaochaguliwa kutoka katika Kata hii isiyo na Shule ya Sekondari | |
| 2 | **Elimu Msingi**<br>Upatikanaji wa Fursa za Uwekezaji katika Tarafa 4 za Halmashauri | i) Mwekezaji anaweza kujenga Shule ya Awali na Shule ya Msingi kwa mfumo wa kiingereza. Pamoja na somo la Kompyuta<br><br>ii) Kuweka miundo mbinu ya Nishati za asili,(mfano gesi na umeme wa Upepo) ambako hakuna miundo mbinu ya nishati , sambamba na miundo mbinu hiyo wawekezaji wataweza kujenga Shule ya Bweni | i) Kupatikana Ajira kwa wananchi wa Manyoni walimu, wafanyakazi wa usafi na upishi pamoja na ulinzi<br><br>ii)Vijana watakaomaliza Shule watakuwa na uwezo wa kutumia Kompyuta katika mifumo ya kielektroniki | |

## 7: SEKTA YA MAJI

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kutunza vyanzo vya Maji vilivyoko katika Halmashauri yetu | Taasisi kuweza kuwekeza katika Miradi ya maji | i) Huduma ya maji kuboreshwa na kuwa endelevu<br><br>ii) Ongezeko la asilimia za upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika | Wananchi wahamasishwe na kuelimishwa juu ya umuhimu wa vyanzo vya maji na athari za mabadiliko ya Tabia Nchi |

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| | | | Halmashauri yetu<br><br>iii) Kupungua kwa magonjwa ya mlipuko yatokanayo na upungufu wa maji safi na salama | |
| | Kutenga eneo kwa ajili ya Maji Taka | Taasisi kuwekeza kwenye Usafishaji wa maji Taka | i) Kuweka Mji katika hali ya usafi na kupandisha hadhi ya Mji<br><br>ii) Kupunguza milipuko ya magonjwa yasababishwayo na uchafuzi wa mazingira | Halmashauri inashauriwa kununua Gari (Bozzer) kwa ajili ya Maji machafu (Taka) |

**8: SEKTA YA AFYA**

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA |
|---|---|---|---|
| 1 | Hospitali ina jengo ambalo likifanyiwa ukarabati linafaa kwa biashara ya chakula, wateja au wagonjwa ni wa uhakika | Mwekezaji anaweza kutoa huduma ya chakula kwa wagonjwa na watumishi ndani ya Hospitali | i) Upatikanaji wa huduma ya chakula kwa urahisi kwa wagonjwa na watumishi<br><br>ii)Kupunguza upotevu wa muda kwa watumishi ambao hulazimika kutoka nje ya uzio kwa huduma ya chakula |
| 2 | Wilaya ina Hospitali na vifaa kwa ajili ya matibabu mbalimbali | Kuanzishwa kwa kliniki binafsi ndani ya Hospitali | i)Kuongezeka kwa mapato ya Hospitali<br><br>ii)Kuongezeka kwa wigo wa huduma kwa wananchi wa Halmashauri ya Manyoni |
| 3 | Uwepo wa Hospitali (Eneo la Mafunzo kwa vitendo) na watumishi wenye taaluma za ufundishaji | Kuanzisha Chuo cha Uuguzi na Utabibu | i) Kupungua kwa tatizo la Watumishi wa Kada za Uuguzi<br><br>ii)Kuongezeka kwa mapato |
| 4 | Ongezeko kubwa la watu katika Halmashauri ya Wilaya | Mradi wa uthibiti wa maji taka (Ununuzi wa gari ya unyonyaji | Kupungua kwa magonjwa ya mlipuko yanayoweza zuilika |

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA |
|---|---|---|---|
| | ya Manyoni na kutokuwepo kwa huduma bora ya unyonyaji wa maji taka | maji taka) | kwa uthibiti wa maji taka |

**9: SEKTA YA MAENDELEO YA JAMII**

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uwepo wa vikundi vya kiuchumi 880 vya ujasiriamali katika Halmashauri ya Wilaya | i) Taasisi za kifedha kuwekeza katika vikundi vya ujasiriamali na VICOBA vilivyopo<br><br>ii) Aidha kuwekeza katika vyama vya ushirika vya kuweka Akiba na Mikopo (SACCOS) | i) Wananchi kupata Elimu ya ujasiriamali<br><br>ii) Kuongeza na kukuza kipato cha Wananchi<br><br>iii) Kuboresha maisha ya wanachama katika ushirika (SACCOS) Kupitia mikopo itakayotolewa | |
| | Uwepo wa NGOs zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya | Kuwekeza katika kuendeleza makundi maalumu yaliyopo katika jamii. Makundi hayo ni yafuatayo (walemavu, wazee, watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi katika jamii) | | |

**10: SEKTA YA ARDHI NA MIPANGO MIJI**

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Uwepo wa njia za usafrishaji, njia za reli na barabara kuu. | Usafirishaji ni chachu katika uwekezaji wa aina yoyote, kwa kuwa zinanampa fursa mwekezaji kusafirisha bidhaa na mali ghafi kutoka pande yoyote ya Tanzania. Pia ni fursa kubwa kwa jamii kuwekeza katika usafirishaji na ufanya | Uwekezaji wa aina yoyote unaoweza fanyika utanufaisha jamii kwa njia ya ajira na upatikanaji wa huduma mbalimbali. | Halmashauri inafanya jitihada katika kutenga maeneo ya viwanda na kilimo kwa ajili ya kuvutia wawekezaji. Pia imetenga Stendi na eneo la kuegesha magari hivyo kuwezesha wananchi |

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| | | biashara ndogo ndogo | | kujiajiri na kuwekeza katika maeneo hayo. |
| 2. | Hekta 899 zimetengwa wa ajili ya uwekezaji wa umeme jua na umeme wa upepo. | Mwekezaji anaweza wekeza mitambo ya kufua umeme wa Jua na Umeme wa upepo katika eneo hilo. | Uwekezaji wa umeme jua na umeme wa upepo utakua chachu ya uwekezaji mwingine kwa ajili upatikanaji wa umeme wa kutosha hiyo upatikanaji wa ajira. | Halmashauri inakaribisha wawekezeji wote wa Umeme wa jua na umeme wa upepo. |
| 3. | Hekta 2309 zimetengwa kwa ajili ya viwanda. | Mwekezaji yoyote anaehitaji kuendeleza au kuanzisha kiwanda cha aina yoyote. | Wananchi watafaidika kwa kupata huduma mbalimbali, ajira na masoko ya mazao yao. | Wawekezaji wanakaribishwa kwa ajili ya kuwekeza viwanda katika Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. |

## 12: SEKTA YA NYUKI

| NA | FURSA ZILIZOPO | UWEKEZAJI AMBAO UNAWEZA KUFANYIKA | MANUFAA YANAYOWEZA KUPATIKANA | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Uwepo wa eneo kubwa lenye uoto wa asili hususani mapori ya miombo (miombo woodland) na vichaka vya Itigi (Itigi thickets) kuruhusu ufugaji wa nyuki wa kibiashara. | Mwekezaji anaweza kuanzisha manzuki/hifadhi za nyuki katika maeneo hayo. | -Kupatikana kwa ajira kwa wakazi wa maeneo hayo.<br>-Jamii kushiriki katika ufugaji wa nyuki.<br>-Kuwepo kwa hifadhi endelevu ya uoto wa asili. | Serikali kuu, Halmashauri, Vijiji na wadau mbali mbali wawe tayari kumpa mwekezaji ushirikiano pale atakapojitokeza. |
| 2 | Utayari wa wananchi kujikita katika ufugaji nyuki bora/kisasa na wafugaji wa jadi kubadilika wakipewa mafunzo stahiki. | Mwekezaji anaweza kuwekeza katika<br>-Kuhamasisha wananchi kujikita katika ufugaji nyuki bora/kisasa kwa kutoa mafunzo/elimu na vifaa stahiki (kuimarisha huduma ya ugani).<br>-Kuanzisha kiwanda cha uchakataji wa mazao ya nyuki. | -Ongezeko la uzalishaji wa mazao ya nyuki yenye ubora unaokubalika katika masoko.<br><br>-Kuwepo kwa ajira na soko la uhakika la mazao ya nyuki (Asali na Nta) karibu na wananchi. | |